

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA TISA

03 JUNI, 2024



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA TISA TAREHE 03 JUNI, 2024

I. **DUA:**

II. **HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA FEDHA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

III. **MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**501. MHESHIMIWA PROF. PATRICK ALOIS NDAKIDEMI (MOSHI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali inatoa mafunzo ya ujasiriamali kwa kiasi gani kwa Vijana kabla hawajapatiwa Mikopo kutoka kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

#### **502. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapandisha hadhi Mji Mdogo wa Mbalizi kuwa Halmashauri ya Mji wa Mbalizi.

#### **503. MHESHIMIWA EDWIN ENOSY SWALLE (LUPEMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali kupitia TARURA ina mpango gani wa kujenga barabara za lami katika Jimbo la Lupembe.

#### **504. MHESHIMIWA NICODEMAS HENRY MAGANGA (MBOGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mkakati gani wa kuwapatia Bodaboda mikopo midogo itakayowasaidia kuwainua kiuchumi.

### **WIZARA YA NISHATI:**

#### **505. MHESHIMIWA MUHARAMI SHABANI MKENGE (BAGAMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Wananchi wa Kata za Yombo na Kiromo wanaopitiwa na mradi wa njia ya umeme kutoka Chalinze hadi Bagamoyo watalipwa fidia.

#### **506. MHESHIMIWA NEEMA KICHIKI LUGANGIRA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali haioni haja ya kupunguza gharama ya gesi ili lengo la asilimia 80 ya Watanzania kutumia nishati safi ya kupikia ifikapo 2033/34 lifikiwe.

### **WIZARA YA KILIMO:**

#### **507. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itajenga mabwawa ya umwagiliaji Kata za Eskesh, Yaeda Chini, Geterer, Gidihim, Maskaroda na Maretadu - Mbulu.

## **WIZARA YA AFYA**

### **508. MHESHIMIWA PRISCUS JACOB TARIMO (MOSHI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kwa nini watu waliopata ajali wanapokwenda Hospitali za Serikali na fomu za PF3 hulipa gharama za kumuona Daktari na kugonga muhuri.

### **509. MHESHIMIWA STELLA SIMON FIYAO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kuna mpango gani wa kupeleka mashine za Watoto Njiti katika Hospitali zote za Mikoa na Wilaya.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **510. MHESHIMIWA SOUD MOHAMMED JUMAH (DONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, kuna mpango gani kufanya mazungumzo ya pamoja kwa upande wa Zanzibar na Tanzania Bara juu ya zuijio la usafirishaji wanyama hai nje ya nchi.

## **WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

### **511. MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali itajenga majengo ya Mahakama ya Mwanzo Ngarenanyuki na katika maeneo jirani ambayo hayana huduma ya Mahakama.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **512. MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, kuna ulazima gani wa Dawati la Kijinsia kuwa ndani ya Kituo cha Polisi.

### **WIZARA YA UJENZI:**

#### **513. MHESHIMIWA MARIAM MADALU NYOKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, kuna mpango gani wa kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Nanjoka – Nalasi - Mchoteke – Njenga – Mjimwema – Magozini - Mtwara Pachani.

#### **514. MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO (BAHI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Bihawana, Mpanga, Chidilo, Chai hadi Manyoni kupitia Itigi kwa kiwango cha lami.

### **WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

#### **515. MHESHIMIWA CONDESTER MICHAEL SICHALWE (MOMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi:-

Je, lini Serikali itajenga Malambo ndani ya Tarafa ya Ndalambo na Msango pamoja na kukarabati Malambo ya Mkomba, Kasanu na Kamsamba.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

*(Majadiliano yanaende/ea)*

**DODOMA**  
**03 JUNI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***  
**KATIBU WA BUNGE**